

Kudhibiti viwavi ambao hukunja majani ya mpunga

Mchele ni chakula kikuu barani Asia lakini huathiriwa na wadudu na magonjwa mengi. Viwavi ambao hukunja majani ni wadudu waharibifu sana wa mpunga ambao huathiri zao katika hatua tofauti.

Usimamizi wa viwavi ambao hukunja majani ya mpunga ni kwa kupanda aina sugu kwa muachano wa 20cm kwa 20cm ili kuruhusu mwanga wa jua kupenya. Tumia mbolea oza kwa sababu nitrojeni nyingi kutoka kwa mbolea za madini huongeza matukio ya wadudu. Tega nondo waliokomaa kwa kutumia mitego ya mwanga, na kuwazuia nondo kuangua mayai kwenye majani. Pia tumia wadudu wenyе manufaa kama vile nyigu ambao huua wadudu waharibifu wa majani. Hawa hutaga mayai yao kwenye mayai ya folda za majani na nyigu anapokua, hula mayai ya folda za mchele na kuyaharibu. Pata kadi zaambazo husana vimelea na kutoka kwa maduka ya pembejeo ya kilimo na uendelee kuzibadilisha kila baada ya siku 20.

Mitego ya mwanga

Mtego rahisi wa mwanga unaweza kufanywa kwa kutumia funeli 2 za plastiki. Kuwa na faneli moja juu ya balbu na nyingine chini ya balbu ili kunasa nondo. Ambatanisha funeli 2 pamoja ukiacha angalau 2cm kati ya funeli hizo. Ambatisha bomba refu la kipenyo cha cm 2.5 kwenye faneli ya chini ili nondo waanguke ndani ya maji. Ambatanisha mtego kwenye ufito wa urefu wa 1.5 m hadi 2m ili mtego uwe juu ya matawi ya mpunga. Ikiwa huna umeme, unaweza kutumia taa ya mafuta ya taa.

Mbinu rahisi za udhibiti

Kuweka vijiti vwenye umbo la T kwenye shamba la mpunga ambavyo huwezesha ndege kutua shambani. Ndege hula viwavi. Unaweza kufungua jani lililokunjwa na kuua viwavi kwa mkono.

Baada ya kuvuna, viwavi hubaki kwenye mabua ya mpunga na magugu. Kuchoma mabua hakuui viwavi waliojificha bali huua wadudu wote wenyе manufaa. Tumia majani ya mpunga kama matandiko kwenye zizi la mifugo, au kama chakula au matumizi

mengine.

Punguza na uondoe magugu ya nyasi kabla ya kupanda mmea unaofuata kwa sababu magugu yanaweza kuficha viwavi. Pia walishé wanyama magugu ya nyasi. Wakati wa ukuaaji wa mazao, ondoa magugu ya nyasi.